

RASIMU 11.5.2020

Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb

HABARI RASMI

Wiki ya Novemba 9-13 itakuwa "Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb" katika Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb (DCSD). Tukio hili la wiki nzima litakuwa na shughuli za mafunzo shulenzi za Black Lives Matter, ikiwemo sherehe za mitandao ya kijamii za Vyuo vya Elimu na Vyuo Vikuu ambavyo Kihistoria ni vya Watu Weusi (HBCUs), adhimisho la biashara zinazomilikiwa na watu weusi katika Kaunti ya DeKalb, Mchuano wa My Brother's Keeper, siku ya "My Black is Beautiful Unity Day," na majadaliano yanayoongozwa na jopo la wanafunzi.

Bodi ya Elimu ilichukua azimio la Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb mnamo tarehe 13 Julai, 2020. Lengo la wiki hii ni kuendeleza harakati inayoendelea kuhusu tafakari muhimu na mazungumzo wazi katika jamii za shule kwa watu wa kila umri kushiriki katika masuala ya haki za kirangi.

"Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb ni wilaya ya shule yenye jamii anuwai na tunasheherekeja jamii hizo anuwai maridadi kwa njia yoyote ile," Msimamizi Cheryl Watson-Harris alisema. "Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb inawapa wanafunzi na wafanyakazi wetu nafasi ya kutambua taswira chanya kwa wanafunzi wetu katika jamii zetu huku tukizungumzia tena dhidi ya udhalimu wa kirangi na kijamii katika jamii zetu."

Black Lives Matter ilianzisha hashtags ya mitandao ya kijamii katika mwaka wa 2013 katika kukabiliana na kuuawa kwa Trayvon Martin aliyekuwa na umri wa miaka 17 na mratibu wa kulinda ujirani kule Sanfrod, Fla. Harakati ya mitandao ya kijamii ilibadilika na kuwa shirika la kimataifa na lengo la kuwezesha nguvu ya kuleta haki, kuponya na uhuru wa Watu weusi duniani kote.

Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb, Bw. Marshall Orson alisema, "Black Lives Matter katika Wiki ya Shule ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb ni thibitisho la ahadi ya Wilaya kwa wanafunzi, wafanyakazi, na jamii zao za umbari. Kwa kuzingatia michango muhimu kutoka kwa jamii hizi, na hata pia changamoto zinazoendelea, tutaboresha maisha ya wale wote ambao ni sehemu au wameguswa na DCSD."

"Katika jamii ya leo, Vuguvugu la Black Lives Matter linawakilisha mwonekano wa yale ambayo mababu zetu walipigania katika historia yote," Mwanachama wa Bodi ya shule Dijion DaCosta alisema. "Mababu wetu walipigania haki, uhuru, usawa, na mageuzi, ambayo yanawafaidi watu walio wachache na watu wasio weupe. Lazima tuendelee kuendeleza historia walioacha kwa kushiriki, kufahamishwa, na kuchagua kuwezesha sauti zetu zisikiike. Sasa ndio wakati wa kubadilisha ujumbe kuwadia mageuzi

yanayoendelea, utofauti, na ujumuishaji. Hatuwezi kujiruhusu kuendelea na tabia hasi za zamani ambazo zinasababisha mgawanyiko. Mabadiliko yanaanza na sisi.”

Kwa maelezo zaidi kuhusu “Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb,” tembelea <https://www.dekalbschoolsga.org/featured-news/black-lives-matter-at-dekalb-schools/>.

Maombi ya vyombo vya habari yanapaswa kutumwa kwa
communications@dekalbschoolsga.org.